

TATHMINI YA ELIMU YA MSINGI YA KENYA
TATHMINI YA DISEMBA 2026
GREDI YA 4 – SHUGHULI YA KISWAHILI



Muda: Saa 2

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: _____

Shule: _____

Nambari ya Tathmini/UPI: _____

Tarehe: _____

Maelekezo kwa Wanafunzi

1. Andika jina lako, Nambari yako ya Tathmini/UPI na tarehe katika nafasi ulizopewa.
2. Kagua karatasi ya maswali kwa makini ili kuhakikisha kurasa zote zimechapishwa na hakuna swali lililoachwa.
3. Jibu maswali yote katika nafasi ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SEHEMU	% YA ALAMA	Kuzidi Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Chini ya Matarajio	Maoni ya Mtaahini
Kiwango		75-100	40-74	21-39	1-20	
Alama						
Kiwango		4	3	2	1	
Weka Alama ya ✓						

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma kifungu kifuatacho. Kimeacha nafasi zilizo na nambari 1–10. Chagua jibu bora zaidi kukamilisha kila nafasi.

Duma ni mnyama ambaye hujulikana kuwa na **(1)** _____ sana. Ni mnyama mwenye mbio **(2)** _____ wanyama wote. Ajabu ni kwamba kila wakati hufaulu **(3)** _____. Duma huwa na mbio katika masafa **(4)** _____. Duma huwa na sura kama ya **(5)** _____. Watalii wanapotembelea mbuga **(6)** _____, huwaona wanyama wengi wa **(7)** _____. Watalii huiletea nchi **(8)** _____ pesa **(9)** _____ za kigeni. Pesa hizo hutumiwa katika **(10)** _____ wa muundo msingi.

- | | | | |
|------------------|----------------|---------------|---------------|
| 1. A. kazi | B. kasi | C. kiasi | D. kashi |
| 2. A. kumliko | B. kuwaliko | C. kuliko | D. kuziliko |
| 3. A. anapowinda | B. alivyowinda | C. alipowinda | D. alikowinda |
| 4. A. madogo | B. fupi | C. mafupi | D. kidogo |
| 5. A. ng'ombe | B. punda | C. chui | D. mbuzi |
| 6. A. zetu | B. letu | C. chetu | D. wetu |
| 7. A. nyumbani | B. shambani | C. porini | D. msituni |
| 8. A. letu | B. wetu | C. chetu | D. yetu |
| 9. A. nyingi | B. mingi | C. wengi | D. mengi |
| 10. A. ubomozi | B. ujensi | C. ujengaji | D. ununuzi |

11. Tambua kitenzi katika sentensi ifuatayo.

Kaka yangu anaandika barua.

A. Yangu B. Barua C. Anaandika D. Kaka

12. Tumia kivumishi kinachofaa kujaza pengo.

Kikombe _____ kimevunjika.

A. Kipya B. Vipya
C. Wazuri D. Ndefu

13. Chagua neno ambalo ni nomino kati ya haya.

Kitunguu, pakua, lake, mwembamba

- A. Kitunguu B. Pakua
- C. Lake D. Mwembamba

14. Maagano kwa mtu ambaye hutarajii kuonana naye tena ni _____.

- A. Alamsiki B. Tuonane kesho
- C. Lala unono D. Buriani

15. Jaza kwa kutumia kielezi kifaacho.

Kobe hutembea _____.

- A. Polepole B. Haraka
- C. Ovyo D. Mno

16. Jibu kitendawili kifuatacho.

Nifungue nikufunike.

- A. Mwavuli B. Mshipi
- C. Macho D. Kivuli

17. Jibu kitendawili kifuatacho.

Ukinitembelea nyayo zi salama.

- A. Sindano
- B. Kaptura
- C. Viatu
- D. Saa

18. Kamilisha sentensi ifuatayo ukitumia kihusishi sahihi.

Chura yumo _____ maji.

- A. Juu ya
- B. Ndani ya
- C. Chini ya
- D. Mfunguni mwa

19. Jaza pengo kwa kihisishi kinachofaa.

_____ Timu yetu imejinyakulia ushindi.

- A. Jamani!
- B. Msalani!
- C. Oyee!
- D. Sokoni

20. Tumia neno la adabu kukamilisha sentensi.

Tafadhali mwalimu, naomba ruhusa kwenda _____.

- A. Chooni B. Msalani
- C. Shuleni D. Sokoni

21. Nomino dereva, kuku na kiwavi ziko katika ngeli ya _____.

- A. A-WA
- B. KI-VI
- C. I-ZI
- D. LI-YA

22. Jaza pengo kwa kiambishi kifaacho.

Ng'ombe yule _____ mekula nyasi zote.

- A. wa B. a C. zi D. ya

23. Mstari mmoja katika ubeti wa shairi huitwa _____.

- A. Mshororo B. Mishororo
- C. Ubeti D. Shairi

24. Kamilisha methali ifuatayo.

Mtoto wa nyoka ni _____.

- A. Nyoka B. Mtoto C. Mayai D. Jinyoka

25. "Kufa moyo" ni nahau yenye maana ya _____.

- A. Kujitahidi
- B. Kupoteza matumaini
- C. Kuendelea sana
- D. Kuwa na kiburi

26. Chagua maneno ambayo yako katika ngeli ya LI-YA.

- A. Gari, yai, joto
- B. Jua, jasho, joto
- C. Mkebe, jasho, jina
- D. Vita, uso, jamii

27. Kipi si chombo cha sebuleni?

- A. Kochi B. Meza ndogo
- C. Susu D. Televisheni

28. Kisawe cha neno *televisheni* ni

_____.

- | | |
|------------|-------------|
| A. Runinga | B. Redio |
| C. Waraka | D. Kompyuta |

29. Kinyume cha neno *maskini* ni _____.

- | | |
|-----------|-------------|
| A. Malkia | B. Mfalme |
| C. Halati | D. Matajiri |

30. Tunasema mfupi kama nyundo na mrefu kama _____.

- | |
|------------|
| A. Twiga |
| B. Mlima |
| C. Sindano |
| D. Korongo |

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 22–31.

Unapotembea mjini, chukua tahadhari kubwa sana. Kuna matapeli wanaohadaa watu mjini. Aidha, matapeli hao hujiweka katika makundi ili kusubiri watembezi wanaoonekana wageni. Pindi wanapowagundua, hunasa pesa, simu na vitu vingine na kukimbia navyo.

Pia kuna wale wanaotumia maneno matamu. Wao hukuandama na ukifika kichochoroni, watakupora na kukimbia. Wengine watakupiga na kukuacha umeumia. Iwapo unataka msaada wowote, basi mtafute bawabu au askari akusaidie. Usijitie kwenye shida tupu bure.

31. Kulingana na taarifa, ni watu gani wanaiba pesa?

- | | |
|-------------|-------------|
| A. Askari | B. Matapeli |
| C. Mabawabu | D. Wakora |

32. Mwandishi anatushauri tufanye nini tunapotembea mjini?

- | | |
|------------------|--------------|
| A. Tujitahadhari | B. Tusiogope |
| C. Tuandamane | D. Tusubiri |

33. Kamilisha methali ifuatayo:

Maneno matamu humtoa _____ pangoni.

- | | |
|------------|-----------|
| A. Sungura | B. Nyoka |
| C. Simba | D. Samaki |

34. Matapeli hao hujiweka kwenye _____ ili kusubiri watu wanaoonekana wageni.

- | | | | |
|---------|----------|------------|-----------|
| A. Gari | B. Umati | C. Makundi | D. Kanisa |
|---------|----------|------------|-----------|

35. Ni watu gani tunashauriwa tuwatafute tunapotaka msaada?

- | | | | |
|---------|-----------|-----------|-------------|
| A. Wezi | B. Askari | C. Walimu | D. Matapeli |
|---------|-----------|-----------|-------------|

36. Mwandishi anatushauri tusijitie kwenye _.

- | | |
|-------------|-------------|
| A. Raha | B. Shida |
| C. Matapeli | D. Magonjwa |

37. Matapeli hao hujiweka kwenye makundi ili kusubiri watu wanaoonekana _____.

- | | |
|-----------|------------|
| A. Walevi | B. Wakora |
| C. Wageni | D. Wajinga |

38. Matapeli wengine hutupiga na kutuacha tukiwa _____.

- | |
|-------------------|
| A. Tunacheka |
| B. Tumeumia |
| C. Tunafurahi |
| D. Tunasherehekea |

39. Taja kinyume cha neno *wageni* kulingana na ufahamu.

- | | |
|------------|--------------|
| A. Wenyeji | B. Watembezi |
| C. Watu | D. Wakora |

40. Ufahamu huu unazungumzia nini?

- | | |
|-----------------|-------------------|
| A. Ujanja mjini | B. Matapeli mjini |
| C. Ujinga mjini | D. Askari mjini |

MAJIBU

Na.	Jibu	Na.	Jibu
1	B	21	A
2	C	22	B
3	A	23	A
4	C	24	A
5	C	25	B
6	A	26	B
7	C	27	C
8	D	28	A
9	A	29	D
10	B	30	A
11	C	31	B
12	A	32	A
13	A	33	A
14	D	34	C
15	A	35	B
16	A	36	B
17	C	37	C
18	B	38	B
19	C	39	A
20	B	40	B